HABARI

Sura za wamachinga wasio raia hatimaye zaadimika Kariakoo

Uk.4



Dkt. Samia alivyoamsha ari ya vijana wa CCM kujiandaa

Uk. 4



CHADEMA WATESWA NA KIVULI CHA CCM

Uk.5

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2521 IJUMAA FEBRUARI 07, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# CCM YAUTIKISA UPINZANI

- **Chadema** wakimbilia Bagamoyo kujitafakari upya
- **Dkt.** Samia, Dkt Nchimbi na Dk Mwinyi ni mlima mrefu kwao
- **Ahadi** ya kuleta wagombea Ubunge imara yawakatisha tamaa
- **Angalizo** la kuwaheshimu lakini kutowaogopa lawapasua vichwa






*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango na Mwenza wake Mama Mbonimpaye Mpango wakitoa heshima za mwisho wakati wa kuaga mwili wa marehemu Sekunda Massawe ambaye ni Mama mzazi wa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda mara baada ya Ibada iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Pius X - Tarakea mkoani Kilimanjaro. Jana Tarehe 06 Februari 2025.*

## Waziri Mkuu ampongeza Rais kuendeleza mahusiano kimataifa

Uk.3



# CCM YATIKISA UPINZANI

NA MWANDISHI WETU

IKIWA imepita siku moja tu imepita tangu Chama Cha Mapinduzi CCM kilipofanya sherehe kubwa za kutimiza miaka 48,, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma upoenda wa upinzani ni kama vile wamemwagiwa maji ya baridi.

Kuanzia juzi Februari 5, hadi hii leo hakuna kiongozi wa chama cha upinzani aliyekuwa tayari kuzungumzia hisia zake baada ya kushuhudia sherehe hizo, pia kusikiliza hotuba ya viongoizi mbalimbali na hasa mgeni rasmi Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan.

Gazeti hili lilitaka kujua kauli za viongozi wa vyama vya upinzani, baada ya kufanyika kwa sherehe za CCM, lakini hakuna chama kilichokubali kutoa ushirikiako huku baadhi ya viongozi wakitoa kauli za hasira wakitaka wasiulizwe masuala yanayohusu chama kingine.

Uchunguzi wa gazeti hili umebaini kwamba sababu za msingi zilizowarudisha nyuma wapinzani ni pamoja na mikakati ya chama hicho tawala hasa safu ya viongozi imara waliosimamishwa na chama hicho kwa ajili ya kugombea nafasi za Urais Tanzania Bara, Mgombea Mwenza na Rais wa Ranzibar. Kukubalika kwa Dkt Samia Rais wa Awamu ya Sita, Uzoefu wa Dkt Emmanuel Nchini ambaye si mgeni katika mizazi ya siasa za Tanzania pamoja na Dkyt Mwinyi anayetamba Zanzibar kwa kuinua uchumi hususan muundo mpya wa Uchumi wa Bluu, amekuwa ni kiongozi anayetarajiwa kukifikisha kisiwa hicho katika nchi ya ahadi.

Ukisikiliza kauli za Mwenyekiti wa Chadema Tundu Lissu hivi karibuni akionyesha nia ya kuwarudisha baadhi ya wanachama waliodaiwa kuasi baada ya kuingia bungeni bila kufuata taratibu, ilionekana wazi alitaka chama chake kiweke nguvu kugombea nafasi za Ubungu, hii inatokana na kuiona nafasi finyu ya kupata mgombea anayeweza kusimama dhidi ya mgombea wa CCM Dkt Samia.

Lakini baada ya hotuba ya jana ya Mwenyekiti wa CCM Dk Samia j0.Baada ya Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kujifungia Bagamoyo kwa 'fungate' ya uponyaji majeraha ya kampeni za Uchaguzi wao uliofanyika tarehe 21 Januari 2025 , leo wameketi Kikao cha Kamati Kuu katika Hoteli ya Millenium wilayani Bagamoyo .ijini Dodoma hasa akisisitiza kuleta wanachama wanaokubalika ili kugombea nafasi za Ubunge na madiwani nao ukawa ni msumari mwingine kwa vyama vya upinzani ambao katika uchaguzi uliopita wa Serikali za Mitaa uliofanyika Mwezi Agosti mwaka jana na hata Uchaguzi Mkuu ulipita nao waliangukia pua.




# WAZIRI MKUU AMPONGEZA RAIS KUENDELEZA MAHUSIANO KIMATAIFA

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa amesema, Serikali itahakikisha inajiimarisha katika kukuza uchumi wake kwa kutumia rasilimali zilizopo ili kuweza kumudu kutekeleza maeneo yote muhimu.

Ameyasema hayo jana Februari 6, 2025 alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbozi George Mwanisongole, katika kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu Bungeni jijini Dodoma.

Mwanisongole alitaka kujua endapo Serikali imejiandaa vipi na mabadiliko ya sera za nje ya nchi ya Marekani ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa sera za Elimu, Afya na Uchumi hususan miradi ya maendeleo inayofadhiliwa USAID.

Akijibu swali hilo Waziri Mkuu alise, kuwa Tanzania ina Uwezo wa Maliasili, kinachotakiwa ni Watanzania kushirikiana kuhakikisha tunatumia Maliasili na Rasilimali tulizonazo ili kujenga uchumi wa ndani na kuwezesha mipango na bajeti iweze kutekelezeka.

Alisema kuwa Tanzania inaheshimu sera za mambo ya nje na inatekeleza mikataba kwa mujibu wa sera hizo kama ilivyokubaliana na nchi husika katika maeneo mbalimbali. "Tumeanza kuona nchi zenye uwezo mkubwa ikiwemo Marekani ikibadilisha sera zao na mabadiliko yake yanathiri baadhi ya nchi, kwetu sisi ni muhimu kuzingatia sera za nje na kuzitekeleza kama tulivyokubaliana."

Pia, Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuifanya Tanzania kuwa na mahusiano na nchi nyingi duniani na Marekani ni moja kati ya nchi hizo.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu ameiagiza Wizara ya Kilimo iendelee kutoa elimu kuhusu uendeshwaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani katika maeneo yote ambayo wanataka mazao yauzwe kwa kupitia mfumo huo ili kuondoa migogoro kwa wakulima.

Ametoa agizo hilo wakati akijibu swali la Mbunge wa Sumve, Kasalali Mageni aliyetaka kufahamu kauli ya Serikali kuhusu taharuki iliyojitokeza baada ya mazao ya choroko kuwekwa katika mfumo wa stakabadhi gharani kwa kuwa zao hilo ni chanzo cha chakula na akiba.

Waziri Mkuu amesema kwenye sekta ya kilimo yapo mazao ya biashara na chakula, pia yapo mazao ya chakula yanatumika kwa biashara, Serikali imeendelea kuimarisha masoko ya mazao kwa kutumia mifumo mbalimbali kufanya biashara za mazao hayo zikiwemo choroko.

Hata hivyo, Waziri Mkuu amesema anatambua yapo baadhi ya maeneo ambayo yana migogoro inayowafanya wakulima washindwe kuamini mfumo huo, hivyo ameiagiza Wizara ya Kilimo kuendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kuondoa taharuki.

Alisema choroko ni miongoni mwa mazao ambayo Serikali imekuwa ikiratibu biashara yake pale ambapo mwananchi ameamua kutumia kama zao la kibiashara kupitia mifumo ya mauzo iliyopo kama kilimo cha mkataba au kuuza mkulima kuuza ndani na nje ya nchi. Waziri Mkuu aliuzungumzia mfumo ambao sasa unatumika kwa mazao mengi kuuzwa kwa minada na inatakiwa iende vizuri, "tuliona tutumie mfumo wa stakabadhi ghalani ambao unawezesha wakulima kupata faida kubwa kutokana na ushindani wa wanunuzi unaofanyika kwa njia ya mnada."

Katika hatua nyingine, Mhehimiwa Majaliwa amesema kuwa Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda ili kuweza kuyanusuru mazao ambayo yanaharibika kwa haraka ikiwemo.

# CHADEMA WATESWA

NA MWANDISHI WETU

UNAUKUMBUKA ule Mkutano Mkuu Maalum wa CCM uliofanyika jijini Dodoma Januari 18 na 19, ambao ulitoka na jina la Makamu Mwenyekiti wa CCM bara, Mzee Steven Wassira na kisha siku ya pili ukaibua majina ya wagombea Urais wa chama hicho Tanzania Bara, ambapo Dkt Samia alipitisha na Dkt Mwinyi akiridhiwa kupeperusha bendera katika uchaguzi huo kisiwani Zanzibar na Dkt Emmanue Nchimbi akateuliwa kuwa Mgombea mwenza wa Urais? basi tukio hilo lilikitesa sana chama cha upinzani Chadema.

Chama hicho kiliamua kupiga hesabu ili kupisha shamrashamra zile za CCM zipite ili wafanye jambo lao la Uchaguzi Mkuu, ndipo wakaamua kuiweka tarehe 21 Januari wakijua cha,ma hicho tawala kitakuwa kimemaliza mkutano wake pamoja na shamra sgamra ambazo kama wasingefanya hivyo zingezima tukio lal kwa nguvu zote.

Hatimauye wakafanya uchaguzi na aliyekuwa Mwenyekiti wake Freeman Mbowe akasalimu amri akiangushwa na Makamu wake Tundu Lissu.

Baada ya kumalizika uchaguzi huo ikachukua muda mtrefu kabla ya Mwenyekiti mpya hajahudhuria katika ofisi za chama hicho zilizopo Mikocheni hadi zilipopita shamra shamra za CCM ndipo naye akapiga hodi ofisini na kusikika akilegeza msimamo wake akiwataka wanachama wote hata wale waliodaiwa kuwa ni waasi ndani chama warejee ili kujipoanga upya.

Juzi Jumatano Kamati kuu ya (CHADEMA) ilikutana katika Hoteli ya Millenium wilayani Bagamoyo, safari hii wakipanga kufanya kikao chao siku moja kabla ya sherehe za CCM zilizofanyika jijini Dodoma, nia ikiwa ni kuhofia kutotulia vizuri kutokana na shamra shamra hizo kufuatiliwa karibu kila kona ya nchi na hata baadhi ya nchi za nje.

Hali hii inaonyesha jinsi chama hicho kinachotishwa na kivuli cha CCM na kiukifanya kipange mambo yake kwa kuangalia kalenda ya matukio ya chama kingine hali inayoonyesha hofu kubwa inayowasumbua kila uchao.

# DART kutumia tikezi za kielektroniki

NA MWA NDISHI WETU

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka DART umesema kuanzia mwezi Machi mwaka huu wa 2025 utasitisha rasmi matumizi ya tiketi za karatasi katika usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka na badala yake watumiaji wote wa Mabasi watatakiwa kutumia kadi janja ambazo zinaendelea kuuzwa katika vituo vikuu vya mradi huo.

Akizungumza Jijini Dar es Salaam wakati wa kuhitimisha mradi wa Maendelezo Yatokanayo na uboreshaji wa usafiri wa umma (TOD), Mtendaji Mkuu wa DART Dkt. Athumani Kihamia amesema ifikapo tarehe mosi mwezi Machi matumizi ya tiketi za karatasi katika kulipia nauli za mwendokasi yatasitishwa.

"Ni kweli tumeendelea kusisitiza watumiaji wa Mabasi yetu ya Mwedokasi wajitahidi kuwa na kadi janja na kuzitumia lakini hata hivyo baadhi yao bado hawatumii kadi hizo, napenda kusisitiza kuwa ifikapo tarehe mosi mwezi Machi mwaka huu tutasitisha kabisa matumizi ya tiketi za karatasi ili wasafari wote wanaotumia Mabasi ya Mwndokasi watumie kadi" Alisema Dkt.Kihamia

Alisema matumizi ya kadi yanaondoa usumbufu wa kukosekana kwa chenchi lakini pia ni njia muafaka ya kudhibiti uvujaji na upotevu wa mapato ya serikali.

Katika hatua nyingine Dkt. Kihamia alisema Serikali imeshaingia mkataba na mtoa huduma ya Mabasi ambaye atatoa huduma katika awamu ya pili ya mradi wa BRT katika Barabara ya Kilwa kuelekea Mbagala hivyo wananchi wa ukanda ho wakae mkao wa kula.

"Mambo ni mazuri sana Serikali sikivu ya Mh.Dkt.Samia Suluhu Hassan imeshafanya jambo lake kuanzia Machi 31 wakazi wa Mbagala na maeneo ya Jirani wataanza kufaidi huduma ya usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka maarufu kama Mwendokasi jambo ambalo wamelisubiri kwa muda mrefu" Alisema.

Aidha Dkt.Kihamia wakazi wa mbagala nao watatumia kadi janja pale huduma itakapoanza ili kuondoa changamoto za mfumo wa tiketi za karatasi kama zilizojiokeza katika awamu ya kwanza ya mradi.

Awali mwakilishi wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEI Mhandisi Gilbert Moga alisema mradi wa TOD japo umekamilika kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake Serikali itaona namna ya kuuendelea kwani ni moja ya mambo ambayo yanaleta tija kubwa katika usafiri wa umma hasa kuleta maendeleo kwa wananchi wa pembezoni mwa mradi.

# PRINCE RAHIM KUMRITHI AGA KHAN

NA MWANDISHI WETU

JUMUIYA ya Waislamu wa Kisheia Ismaili imemtangaza Prince Rahim Aga Khan V kama Imamu wa 50 wa urithi wa Waislamu wa Kisheia Ismaili, kufuatia kifo cha baba yake Aga Khan IV, aliyefariki dunia mjini Lisbon akiwa na umri wa miaka 88.

Mpito huu unaendeleza ahadi ya kudumu ya Imamu wa Ismaili kwa maendeleo ya kibinadamu, ambayo imekuwa nguzo muhimu ya kazi iliyofanywa chini ya uongozi wa Aga Khan IV ambaye katika uongozi wake wa miongo kadhaa, alijitolea kuboresha hali ya maisha duniani kote, kwa msisitizo maalum barani Afrika, Asia, na maeneo mengine yanayohitaji miradi ya maendeleo.

Kupitia Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), aliongoza upanuzi wa miradi inayolenga kuimarisha elimu, huduma za afya, maendeleo ya uchumi, na uhifadhi wa utamaduni katika mabara mbalimbali Afrika, hususan Tanzania, Kenya, Uganda, na Msumbiji, imekuwa eneo la kipaumbele kwa uwekezaji mkubwa katika shule, vyuo vikuu, hospitali, huduma za kifedha, na maendeleo endelevu yanayolenga kuleta mabadiliko ya muda mrefu.

Dira ya Kuendeleza na Kupanua Miradi

Chini ya uongozi wa Aga Khan V, Imamu wa Ismaili amethibitisha dhamira yake ya kuhakikisha kuwa miradi na programu zote zilizoanzishwa na Aga Khan IV zinaendelea na kuimarishwa zaidi.

"Kwa muda mrefu, Prince Rahim Aga Khan V amehusika kikamilifu katika uongozi wa AKDN, akiwa na mchango mkubwa katika mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira, na kupunguza umaskini".

Uwepo wa AKDN nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla unasalia kuwa sehemu kuu ya dhamira yake, kupitia miradi inayoendelea ambayo inajumuisha:

Kuongeza upatikanaji wa elimu bora kupitia Shule za Aga Khan na vyuo vikuu vya Aga Khan Afrika Mashariki, kuimarisha mifumo ya afya na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kisasa za tiba kupitia Aga Khan Health Services (AKHS).

Miradi mingine ni kuhamasisha maendeleo ya uchumi kwa kusaidia ujasiriamali na miradi ya kifedha kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Aga Khan (AKFED) na kuimarisha uendelevu wa mazingira, kwa kuendeleza miundombinu rafiki kwa mazingira na programu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Jumuiya ya Ismaili inaposherehekea urithi wa Aga Khan IV, Imamat inaingia katika enzi mpya ya uongozi, ikiendeleza ahadi yake ya kuimarisha maendeleo ya kijamii, ustawi wa binadamu, na maendeleo endelevu kwa jamii zinazoihitaji zaidi.

Prince Rahim Aga Khan V ni mtoto wa kwanza wa Aga Khan IV, Amezaliwa tarehe 12 Oktoba 1971, amesoma katika Phillips Academy Andover na Chuo Kikuu cha Brown, na amehudumu katika bodi mbalimbali za AKDN, akiongoza pia Kamati ya Mazingira na Tabianchi, kwa kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo inaendana na malengo ya uendelevu wa muda mrefu.



# SURA ZA WAMACHINGA WASIO RAIA HATIMAYE ZAADIMIKA KARIAKOO



NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, ameunda kamati maalumu ya watu 15 kuchunguza wingi la wageni kufanyabiashara za uchuuzi 'Umachinga' katika eneo la Kariakoo, Dar es Salaam.

Hatua hiyo inatokuja baada ya mwishoni mwa wiki, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kusikia kilio cha Watanzania hususan wafanyabiashara wa Kariakoo, kuhusu kero hiyo.

Dk. Jafo alisema kamati hiyo itakayokuwa chini ya Mwenyekiti wake, Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Profesa Edda Lwoga, itafanya kazi hiyo ndani ya mwezi mmoja na kuwasilisha taarifa yake.

Alitangaza hayo, jijini Dar es Salaam, jana, alipokutana na wafanyabiashara wa Kariakoo akiwemo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe, Mwenyekiti wa Soko la Kariakoo na Halmashauri Kuu ya uongozi wa soko hilo.

"Hivi karibuni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokea kilio cha wananchi wa Kariakoo, Dar es Salaam na Watanzania hususan wafanyabiashara, suala la hivi sasa kuwepo kwa mwingiliano wa wageni wengi ambao huwa wanakuja na ajenda ya uwekezaji, kwa bahati mbaya uwekezaji wao hauakisi suala zima la uwekezaji," alisema.

"Wanapofika nchini changamoto iliyojitokeza ni kwamba, wanashiriki katika shughuli nyingine ambazo zipo nje ya utaratibu wa uwekezaji," alisema.

"Baadhi ya shughuli hizo hususan ni kufanya biashara za rejareja za kimachinga, mwisho wa siku huathiri mwenendo wa biashara kwa Watanzania," alisema.

Waziri huyo alisema hiyo imekuwa kero kubwa kwa wafanyabiashara na kuathiri biashara zao huku ikizingatiwa Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni ambapo mgeni yoyote au mtu anapaswa kufanyabiashara kulingana na maelekezo ya serikali.

"Kuna wingi la wageni ambao wanafanya biashara tofauti na utaratibu wa kisheria, hivyo huleta kero kwa wafanyabiashara wazawa na kuathiri mitaji yao na kuwa na vijana waliofilisika kutokana na wengine wameanzisha magodauni na kuleta biashara na kuuza rejareja," alisema.

Alisisitiza kuwa, jambo hilo halivumiliki, hivyo anatekeleza maelekezo ya Rais Dk. Samia akiwa waziri mwenye dhamana kwa kuunda kamati maalumu ya watu 15, kuondoa changamoto hiyo inayowakabili wafanyabiashara.

Dk. Jafo alisema Mwenyekiti wa kamati hiyo, Profesa Edda anaamini atasaidia kwa kuwa amebobea upande wa biashara, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa wizara hiyo, Sempeho Manongi (Katibu wa Kamati).

Wajumbe ni Naibu Kamishna wa Polisi, Francis Maro, Naibu Kamishna Uhamiaji, Kigongo Shile, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Latifa Khamis.

Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Godfrey Nyaisa, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya ushindani nchini (FCC), William Erio, Teddy Frank, Zubeda Masoud, Ofisa Kazi Mwandamizi wa Dar es Salaam, Eliuluma Mabelia, Raphael Maganga kutoka sekta binafsi, Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Kariakoo, Severine Mushi na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe.




Alitaja miongoni mwa hadidu za rejea ni utafiti wa kina Soko la Kariakoo likiwa kama la mfano, kubaini ukubwa wa tatizo la wageni kufanya biashara nchini ambalo linaathiri ajira kwa Watanzania.

Pia watakagua vibali vya wageni na uhalali wake, kuchunguza wageni kupewa vibali na leseni za biashara zinazofanywa na Watanzania.

Dk. Jafo alisema kamati hiyo itaangalia masuala ya dharura ni nini kifanyike kwa haraka kutatua tatizo hilo kwa kuainisha njia za haraka na muda mfupi, chanzo cha tatizo na namna ya kuepuka.

Aliwaomba wafanyabiashara kuwa watulivu wakati kamati hiyo inafanya kazi yake ambayo itasaidia siyo tu sekta ya biashara bali na nyingine kuweka misingi ya utekelezaji.

# SERA MPYA YA ELIMU YAWEKEWA MIKAKATI

NA MWANDISHI WETU




KATIKA kutekeleza Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la Mwaka 2023, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imetenga shilingi bilioni 3 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu na vifaa mbalimbali vya mafunzo ya amali kwa shule 20 nchini.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Erasmus Kipesha, ameyasema hayo katika banda la TEA alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla ya uzinduzi wa sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 iliyozunduliwa na Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Dkt.Kipesha amesema kuwa wajibu wao ni kuhakikisha wanaunga mkono utekelezaji wa Sera hiyo ya Elimu kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa maana ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara za Sayansi, nyumba za walimuna vifaa mbalimbali vya mafunzo ya amali kama michezo, ushoni, mapishi, kilimo, sanaa na TEHAMA

Aidha amesema kuwa watahakikisha wanaimarisha miundombinu ya elimu kote nchini kuunga mkono utekelezaji wa sera ya elimu kwa kuwa na miundombinu na vifaa vya mafunzo ya amali.

"Jukumu letu kubwa ni kuimarisha na kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia kwa kujenga vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu, maabara, mabweni pamoja na kuweka vifaa mbalimbali vya elimu vya mafunzo ya amali.

"Kwa sasa tumetenga shilingi bilioni 3 kwa ajili ya miundombinu ya amali kwenye shule 20 hapa nchini pamoja na vifaa mbalimbali vya amali ambavyo vitakuwa mkombozi na kuchochea kukua kwa elimu bora na ya kiwango"amesema Dkt. Kipesha

Akizungumzia sera mpya ya elimu Dkt.Kipesha, amesema kuwa elimu ya Tanzania sasa inaenda kuwa elimu ya kimataifa zaidi na itakayowapeleka vijana wengi katika soko kwani vijana wengi watakuwa na elimu pamoja na ujuzi.

Hata hivyo ameeleza kuwa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuwakomboa vijana wa Kitanzania kwa kuboresha sera ya elimu na mafunzo ambapo vijana wengi wataweza kujiajiri au kuajiriwa mahali popote nchini kulingana na ujuzi watakaoupata mashuleni.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# TAFAKURI ZINAZOBADILIKA INAPOKUWA SIFA YA UPINZANI NCHINI

NA SWALEH MAOUS AKHERY, PEMBA

MARA nyingi katika siasa za Tanzania hasa kwa vyama vya upinzani, viongozi wake wamekuwa wakicheza sana na hisia za watu, kuwa ili mwanasiasa apate wafuasi basi ajifunze kukebehi na kusema vibaya kazi inayofanywa na serikali.

Lakini katika hali isiyokuwa ya kawaida kauli zao za kuponda, huwa hazidumu wanaweza asubuhi wakalaumu hili na jiuoni wakalipongeza, ndiyo aina ya siasa zinazowapa kiki wanasiasa wa upinzani.

Hata sehemu iiliyojengwa daraja wakisema kuwa hapana kitu pale ilimradi wasikilizaji wanashangilia hayo ndiyo mafanikio ya siasa za upinzani za Tanzania, bahati njema Watanzania sasa wamepata weledi wa kufanya tathmini kabla ya kuamua kufanya jambo lolote.

Wananchi sasa wanasikiliza na kufanya upembuzi, ndiyo maana haitokei kama ilivyokuwa miaka ya nyuma wakati nchi hii ilipoanza kuingia katika mfumo wa vyama vingi ambapo ilifikia watu wakitakiwa waandamane wanafanya hivyo bila hata kuulize pengine sababu au wanatoka na kwenda wapi na kudai jambo gani na kwa nani.

Januari 17 mwaka huu wakati akizungumza katika mdahalo wa kisiasa, Tundu Lissu alisema, yeye ndiye niliyekuwa wa kwanza, kupuliza filimbi kwamba kuna rushwa kwenye chaguzi zetu (Chadema). tena akisisitiza kuwa muda huo alipokuwa akizungumza, walikuwepo wajumbe waliokuwa wakisafirishwa na kuwekwa kwenye mahoteli, makambi, kisha wanapewa pesa, na kulishwa na wagombea, ambao hakuwataja, lakini muda mfupi baada ya kura kutangazwa na yeye kutangazwa mshindi, akatoa kauli ya kushukuru akisema uchaguzi ulikuwa huru na haki!.

Hili ni tatizo ambalo wakati fulani huko nyuma lilizungumzwa pia. Mwezi Mei 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (Takukuru), ilitangaza kuanzisha uchunguzi kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya fedha ndani ya Chadema.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo aliwahi kusikiliza madai ya rushwa katika chama hicho naye akasisitiza kuwa "kwa mujibu wa taarifa alizokuwa nazo, kuna matumizi mabaya ya fedha za michango ya wanachama, ambayo kwa mujibu wa katiba yao wanadai imeanishwa wachangie. Lakini, matumizi yake ndio wanatilia mashaka, kuna fedha nyingi zinatumika ndivyo sivyo, nje ya makubaliano yao. Kwa hiyo, tunachunguza matumizi yasiyo sahihi ya fedha zao."

Ikiwa ufisadi ama rushwa ni tatizo ambalo lipo ndani ya Chadema na lipo kwa muda mrefu, ni matarajio ya wengi kwamba hii itakuwa ni kazi nyingine kubwa ambayo Lissu inamngoja mbele yake.

Uhusiano wa upinzani na serikali

Moja ya hoja ambayo Lissu ameitumia kumkosoa Mbowe, ni namna alivyokuwa akiendesha siasa zake na serikali. Kwa lugha nyingine, Lissu alimwona Mbowe amekuwa laini mbele ya chama tawala na serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Mwenyekiti aliyekwenda gerezani, si mwenyekiti aliyetoka gerezani miezi minane baadaye. Yule aliyetoka gerezani alikuwa tofauti, akiimba maridhiano anaimba mapendano," alisema Lissu.

Alipoulizwa na BBC juu ya mwelekeo wake mpya wa kisiasa na utakuwa na tofauti gani na hali ya sasa. Tundu Lissu amesema:

"Ni mwelekeo wa harakati za mapambano ya demokrasia, hakuna tena kuimbiana habari ya maridhiano yasiyokuwepo, hakuna habari ya kualikana kuzungumza mambo yasiyojulikana. Nia mapambano ya kudai mabadiliko. Na zitakuwa ni siasa za mshike mshike kweli kweli. Ndio historia ya mapambano ya kidemokrasia ilivyo dunia nzima."

Chadema kama vilivyo vyama vingine vya upinzani, inapigia upatu kuwepo kwa katiba mpya, tume huru ya uchaguzi, inataka uchaguzi huru na haki mwishoni mwa mwaka huu, bila ya wagombea wao kuenguliwa bila sababu za maan, pia inataka viongozi na wafuasi wake wasibughudhiwe na vyombo vya dola wanapokuwa kwenye shughuli zao za kisiasa.

Katika nchi yenye demokrasia inayoeleweka, yumkini hayo sio mambo ambayo utawala unapaswa kuyatoa kama huruma kwa vyama vya siasa, ni mambo ambayo yapo kikatiba na kisheria, bahati mbaya utawala nchini Tanzania – kama ilivyo kwa tawala nyingine nyingi duniani – hautendi haki wakati wote. Kuna nyakati za vuta ni kuvute, pingu kiunoni na kirungu mkononi.

Maswali yanayoibuka kwa muktadha huo Je, Chadema chini ya Lissu itahitaji kuwa na uhusiano au ushirikiano na utawala ili kuyafanikisha hayo? Au ina uwezo wa kuyafanikisha bila ya mwingiliano wowote na upande wa serikali?

Lissu baada ya kuibuka na ushindi alianza hotuba yake kwa kusema, atazungumza kwa kuchagua maneno yake kwa uangalifu, na kweli akafanya hivyo. Je, tutarajie Lissu ambaye ataendelea kuchagua kauli zake hata akiwa katika harakati dhidi ya chama tawala na serikali yake?



# TAHARIRI

## Kwa hili CCM inastahili pongezi

WANACHAMA wa Chama Mapinduzi (CCM), sambamba na wananchi wote Tanzania wametakiwa kuwa makini na viongozi wenye tabia ya uchonganishi kwa kile walichodai baadhi yao kuchochea chuki inayoweza kuwatenganisha.

Hiyo ni kauli makini iliyotolewa na katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa ndugu Amos Makalla wakati akizungumza na Wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Viwanja vya Umoja ni nguvu kusini Pemba ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya Mikoa 6 Visiwani Zanzibar.

Makalla pia amesema kuwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt Hussein Mwinyi hawana ubaguzi wowote kwenye suala la kuwaletea maendeleo lakini wenzetu kila kukicha wanaweka fitina na hili kazi kwenu Wazinzabar kwa ujumla wakataeni Viongozi hao na wanasiasa hao kwa kuwanyima kura wakati Uchaguzi utakapofika na tuchague chama cha mapinduzi ambacho ndio kina wajibu wa kuyaleta.

Kauli hii haistahili kupita bila kupongezwa ndiyo maama sisi JAMVI LA HABARI tunaipongeza kwa vile imezingatia kuleta umoja mshikamano na maelewano baina ya Watanzania.

Tunasema hayo tukijua kwamba kipindi kijacho yani Mwezi Oktona nchi itaingia katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na Madiwani hivyo wasioitakia mema nchi wanaweza kutumia nafasi hiyo kuingiza chuki na hasama baina ya wananchi.

Tunaamini kila aliyesikia rai hii iliyotolewa na chama tawala, atazingatia kwa vile nchi hii ina wanasiasa na wasio wanasiasa ambao wanahitaji amani na utulivu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778, - 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684, - 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango akimfariji Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda kufuatia kifo cha Mama yake marehemu Sekunda Massawe wakati alipowasili nyumbani kwa familia hiyo Kijiji cha Nduweni Tarakea Wilayani Rombo Mkoani Kilimanjaro, jana.*

UCHAMBUZI

# Ushindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi waliibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# Dkt Samia alivyoamsh

NA MWANDISHI WETU



VIJANA wanaounda Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), labda sasa washindwe wenyewe kutekeleza majukumu yao kwa vile Mwenyekiti wa Chama hicho na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kueleza dhamira ya chama hicho kikongwe kuwapa kipaumbele ili waweze kuwa imara zaidi na kuongoza katika maeneo mbalimbali ya kisiasa au serikalini.

Katika hotuba yake ya kilele cha sherehe za CCM kutimiza miaka 48 zilizofanyika juzi jijini Dodoma, Mwenyekiti huyo alieleza dhamira ya dhati ya kuwapoa kipaumbele vijana kama maandalizi ya kupata vionhgozi imara wa kesho, huku akitoa mfano kwa makada wakongwe wa chama hicho waliokuwepo katika sherehe hizo, Dkt Jakaya Kikwete aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho na Rais wa Awamu wa nne na hata Makamu Mwenyekiti wa chama hicho bara Mzee Steven wassira kuwa wamepatikana kutoikana na malezi waliyoyapata enzi ya vyama vya TANU na baadaye CCM.

MKatika mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi chote alikiri kuwa CCM ni chama imara na kina mtaji mkubwa wa wanachama ambao mpaka sasa wanafikia Milioni 12 pamoja na wapenzi wengi, lakini alisisitza kuwa hiyo isiwe sababu ya kubweteka kwa mafanikio hayo na badala yeke wanatakiwa kupambana ili kuwatumikia Watanzania ili waione thamani ya chama kilichopewa ridhaa ya kuongoza Serikali yao.

"Tunataka watupime kwa tunachokifanya leo, watuchague kwa sera pamoja na mipango mizuri" alisema Dkt Samia huku akishangiliwa na umati wa Wana CCM pamoja na wapenzi wa chama hicho waliohudhuria sherehe hizo.

Dodoma, tarehe 5 Februari 2025

Mwenyekiti huyo aliahidi kuwa CCM italeta wagombea wanaokubalika na wananchi katika Uchaguzi Mkuu wa 2025, ili kurahisisha uchaguzi wa diwani, mbunge na rais kutoka chama hicho.

Akizungumza katika kilele cha sherehe za miaka 48 ya CCM, zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, Dkt. Samia alisisitiza kuwa mchakato wa kupata wagombea utazingatia haki na uwazi, kwa kushirikiana na viongozi wenzake ndani ya chama.

"Nawahakikishia wana CCM na Watanzania kwa ujumla kuwa, tutahakikisha haki inatendeka katika mchakato wa kupata wagombea wa CCM. Lengo letu ni kuleta wagombea wanaokubalika, ili kuwapunguzia wananchi changamoto ya kuchagua mafiga matatu, Diwani, Mbunge, na Rais," alisema huku akishangiliwa na maelfu ya wananchi.

Kwa upande wa Zanzibar, alieleza kuwa mwelekeo huo utahakikisha upatikanaji wa diwani, mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa mujibu wa taratibu za chama.

Aidha, Dkt. Samia aliwataka wanachama wa CCM kujipanga kikamilifu kwa uchaguzi wa 2025 na kuepuka kubweteka, akiwahimiza kushiriki kikamilifu katika kampeni za chama na kutowabeza wapinzani.

Katika hotuba yake, pia aliwahimiza vijana na wananchi wote kuhakikisha wanajiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili waweze kushiriki katika uchaguzi.

Akihitimisha, Dkt. Samia aliwashukuru wana-CCM kwa imani waliyoonesha kwake, Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuwachagua kupeperusha bendera ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa 2025, akisisitiza kuwa chama kitaendelea kuwa chaguo la wananchi kwa misingi yake ya haki na utumishi wa watu.

Vilevile katika hotuba yake Mwenyekiti huyo ametilia ml zo kuimarisha Jumuia ya vija UVCCM, ambao ameitaja ku ndiyo itakayojenga chama ima kwa kuandaa viongozi waj wataokiendeleza chama hic na baadaye kushika hatamu uongozi.

Kuhusu Ajira kwa vijana D Samia alisema, tayari wamea za kuboeresha Sekta ya Elim wezeshi ambayo inatoa fur kwa vijana kusomea mafun ya ufundi ili waweze kujia pamoja na kuajiri wenzao, masuala ya utalii, Uchumi

# ...a ari ya vijana wa CCM



Naye Katibu Tawa la wa Wilaya ya Namtumbo Fransis Mgoloka alisema,katika kipindi cha miaka minne Wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh.bilioni 46.554

ka-
na
wa
ara
jao
ho
za

Okt
an-
mu
rsa
azo
jiri
pia
wa

Bluu pamoja na elimu ni miungoni mwa mambo yanayotiliwa mkazo ili kuwakomboa vijana katika tatizo kubwa la ukosefu wa ajira linaloikumba dunia hivi sasa.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA, mwenyekiti huyo alisisitiza matumizi ya teknolojia hiyo kwa maendeleo, huku akitoa mfano jinsi yeye mwenyewe alivyoweza kuwatumia ujumbe wanachama wengi akiwataka wajitokeze kwenda kupiga kura katika uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika nchi nzima

Mwezi Agisti mwaka jana na kufanikisha chama chake kushinda kwa kishindo.

Sherehe kama hizo pia zilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini, huku Wana CCM wakijipongeza kwa kuwa ni chama imara kinachoendelea kuaminiwa na wananchi na kushika Dola kwa miaka mingi.

Awali Makamu Mwenyekiti Mzee Steven Wasira akizungumza katika sherehe hizo alisema, CCM kinaendelea kuongoza kutokana na kupata ridhaa ya Watanzaniua, hivyo amewataka wale wanaosema chama hicho kimekaa sana madarakani, waeleze kama kuna ahadi au mipango ya muda ambayo walikaa na kupangiana kutawala kwa zamu.

Alisema tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea heshima.sayansi, mabweni,miundombinu ya vyoo na maji kwenye shule za Sekondari na Sh.bilioni 2,545,934,950.50 zimetumika kujenga miundombinu kama hiyo katika shule za msingi.

Katika sekta ya afya alisema,wamepokea Sh.bilioni 3,155,923,169.67 kujenga zahanati,vituo vya afya,nyumba za Watumishi, miundombinu ya vyoo na maji na Sh.bilioni 1,106,017,026.21 zimetumika kwenye mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia mapato ya ndani(mikopo ya asilimia kumi).

Aidha, Halmashauri ya Wilaya imetumia Sh.bilioni 11,346,151,952 kuwezesha mpango wa kunusuru kaya maskini(Tasaf) ,elimu bila malipo kwa shule za Sekondari,ujenzi wa miundombinu shule za msingi(BOOST)na pembejeo za kilimo.

Alisema,Wakala wa maji na usafi wa mazingira vijijini(Ruwasa) umepokea Sh.8,271,911,919.52,TARURA Sh.bilioni 10.500,Mamlaka ya maji Tunduru mjini Sh.bilioni 3.9,Tanesco Sh.bilioni 10.490,umeme vijijini(REA)Sh.bilioni 11.984 na miundombinu ya umeme Imara Sh.bilioni 245.980.

Naye Katibu Tawa la wa Wilaya ya Namtumbo Fransis Mgoloka alisema,katika kipindi cha miaka minne Wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh.bilioni 46.554 kati ya hizo Sh.bilioni 3.351 zimekwenda kwenye sekta ya afya,elimu Sh.bilioni 9, Sh.bilioni 8 umeme vijijini(REA) na sekta ya maji Sh.bilioni 7.8.





# SERIKALI YATAKIWA KUJADILI UAMUZI WA TRUMP



NA MWANDISHI WETU

SERIKALI imeshauriwa kutenga bajeti ya ziada kugharimia programu zilizokuwa zikifadhiliwa na serikali ya Marekani ili wananchi wasikose huduma zikiwemo za afya.

Aidha, Bunge limeombwa kujadili kwa dharura uamuzi wa Serikali ya Marekani wa kuzuia misaada kwa nchi masikini ikiwemo ya afya na liishauri serikali kwa manufaa ya nchi.

Mhadhiri kutoka Shule ya Biashara Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Omary Mbura amesema taifa linapaswa kutafuta njia mbadala kugharimia huduma zikiwemo za afya ziendelee kupatikana miongoni mwa wananchi.

Profesa Mbura amesema serikali inapaswa kugharimia au kupata dawa hizo kutoka sehemu nyingine na iwatoe hofu wananchi hususani wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU).

Mchambuzi wa masuala ya uchumi, Walter Nguma amesema nchi za Afrika zinapaswa kuwa na bajeti inayokidhi mahitaji ya kununua afua za afya kwa kutumia rasilimali zao.

"Hatua ya Marekani itutoe usingizi Waafrika, tunategemea hadi chandarua, hii ni aibu na tutegemee kupata manyanyaso. Tuanze kutekeleza dhana ya kujitegemea kwa vitendo na si maneno," amesema Nguma.

> "Ukimwi upo, polio, kifua kikuu, matende vyote vipo ila tu havionekani kutokana na kinga na tiba tulizokuwa tunapata kwa hiyo serikali ione itasaidia vipi wananchi wake,

Amesema ni muhimu Bunge la Tanzania likajadili suala hilo kwa sababu kama nchi haikuwa na bajeti ya kununua dawa liishauri serikali jambo la kufanya.

"Suala hili lichukuliwe kwa udharura wake kwa kutenga bajeti itakayokuwa maalumu kwa ununuzi wa dawa na si kuendelea kutegemea misaada inayotufanya kuwa watumwa, badala yake tuone ni jukumu letu hata kama watabadili maamuzi," amesema Nguma.

Mchambuzi wa uchumi, Gabriel Mwang'onda amesema kama Tanzania ilivyoweza kutoa huduma ya usambazaji umeme katika vijiji vyote kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na bila kutegemea ufadhili, inaweza kusimama yenyewe na kupata dawa hizo.

"Wizara ya Afya ina dawati la dawa za asili, ni wakati wa kutoa fedha kwa watafiti wetu waweze kufanya utafiti kupata dawa za asili ambazo zitatumika kufubaza VVU na kutibu malaria badala ya kutegemea dawa kutoka nje," amesisitiza mchambuzi huyo wa uchumi.

Mchambuzi wa masuala ya diplomasia, Goodluck Ng'ingo amesema uamuzi wa Marekani unazikumbusha nchi za Afrika umuhimu wa kuwa na viwanda vya kutengeneza dawa.

"Kwa sababu ARVs hazitengenezwi Marekani, zinatengezwa India, Marekani wanasaidia kutoa fedha kuzinunua kwa ajili ya nchi masikini ambazo zina uwezo wa kutengeza viwanda," amesema Ng'ingo.

Dk Cecilia Makafu amesema ni wakati wa serikali kufanya jitihada za haraka kunusuru hali hiyo kabla ya madhara kuwapo.

"Tatizo lipo kweli kwa maana baada ya zile dawa za akiba ambazo huwa zinakuwepo, kwa kawaida zikiisha maana yake ugonjwa utafumuka, kama tulikosea mwanzo basi tuangalie tulipoishia turekebishe," amesema Makafu.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya amehimiza serikali kufanya jitihada kunusuru afya za wananchi.

"Ukimwi upo, polio, kifua kikuu, matende vyote vipo ila tu havionekani kutokana na kinga na tiba tulizokuwa tunapata kwa hiyo serikali ione itasaidia vipi wananchi wake," amesema Sakaya.

Aliongeza: "Tulishasahau kama kuna Ukimwi tukawa tunashughulika na magonjwa mengine ambayo kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa, sasa turudi tena kwenye kupambana na huu ugonjwa tusisubiri mpaka vifo. Hii ni kengele tufanyie kazi," amesema.

Takwimu zinaonesha Ukimwi bado ni tatizo duniani. Kwa mujibu wa WHO, hadi mwishoni mwa 2023, watu milioni 39 duniani walikuwa wanaishi na VVU.

Atakuwa mkubwa zaidi kama atapata wasimamizi sahihi wa kazi zake, unaweza kuwa na kipaji kikubwa sana ila usipopata watu sahihi ni kazi bure.



# MKUTANO WA NISHATI AFRIKA UNAENDELEA KUIFAIDISHA NCHI



NA MWANDISHI WETU

BAADA ya kufanyika Mkutano Mkuu wa Nishati wa nchi za Afrika na kuhudhuriwa na zaidi ya wakuu wa nchi 23 chini ya wenyeji wa Tanzania na kupata mafanikio makubwa, pongezi mbalimbali zimeendelea kutolewa huku nchi ikizidi kupata faida ya kufunguka kiuchumi katika nyanja mbalimbali ukiwemo utalii.

Bunge la Tanzania ndiyo liliiloanza kutoa Azimio la Kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Nishati Afrika (Misheni 300) hapa nchini.

Hatua hiyo ilitangazwa Spika wa Bunge Dk Tulia Ackson, alipotangaza rasmi kwamba Bunge limepitisha azimio hilo baada ya kuwahoji wabunge wote kwa umoja wao bila tofauti za kivyama walilikubali azimio hilo.

Akisoma azimio hilo mbele ya Bunge, mbunge wa Viti Maalumu, Asia Halamga (CCM) alisema bunge hilo katika mkutano wa 18, kikao cha Nne, Januari 31, 2025, linaazimia kwa dhati na kauli moja kumpongeza Rais Samia kwa kuwa mwenyeji na kufanikisha mkutano wa nishati wa Afrika wa mwaka 2025 kwa weledi na viwango vya kimataifa.

Pia, alisema azimio hilo linampongeza Rais Samia kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo 2030 Watanzania wote watakuwa wamefikiwa na miundombinu ya umeme.

Alisema pia, kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa ifikapo 2030 asilimia 75 ya Watanzania watakuwa wamepata nishati safi ya kupikia na hatimaye kufikia 2034 Watanzania wote wawe wamepata nishati safi ya kupikia.

Vilevile, alisema Azimio hilo linamuunga mkono Rais Samia katika dhamira yake ya kuwapatia Watanzania wote nishati ya umeme na nishati safi ya kupikia.

Katika mkutano huo uliofanyika Januari 27 hadi 28, 2025 ulikuwa na manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi na Afrika.

Alitaja manufaa hayo kuwa ni kwa wawekezaji katika sekta ya hoteli na malazi, usafiri na usafirishaji, wauzaji wa vyakula na vinywaji, bidhaa mbalimbali na sekta ya utalii.

Kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano, alisema wafanyabiashara wametengeneza mtandao katika biashara zao kwa kufanya mazungumzo ya kibiashara pembezoni mwa Mkutano huo.

Halamga alisema kupitia mkutano huo pia, nchi imeingiza fedha za kigeni suala ambalo limeleta manufaa makubwa kwa uchumi.

Rais Samia akifungua mkutano huo alisema, "Mkutano huu unazungumzia zaidi ya nishati, ni kuhusu kuzipa nguvu familia, kuinua mamilioni ya watu kutoka kwenye umasikini na kuleta matumaini na fursa kwa vijana. Ni ahadi yetu

kuwa, mabadiliko ya kiuchumi, kukuza viwanda, kuunda ajira na kuchochea uvumbuzi Afrika."

Wazo la kumpongeza Rais Samia, liliibuliwa na Umoja wa Wabunge Wanawake (TWPG) chini ya Mwenyekiti, Shally Raymond, makamu Sofia Mwakagenda na Katibu Agnes Hokororo na kujadiliwa na bunge lote na kupitishwa.

Wakichangia Azimio hilo mbunge wa Singida Mashariki, Elibariki Kingu (CCM) alisema Afrika ina watu bilioni 1.5 ambao asilimia 60 ni vijana chini ya miaka 25, hivyo mipango hiyo itasaidia kuleta ajira kwa vijana milioni 185 kupata ajira.

Naye, Mbunge wa Kuteuliwa Shamsi Vuai Nahodha (CCM), alisema Rais Samia amekuwa kinara wa kutetea masuala ya msingi kwa binadamu, ikiwemo nishati safi.

Mbunge wa Viti Maalumu, Jesca Kishowa (CHADEMA) alipongeza Mkutano Mkuu wa CCM kwa kumteua, Samia kuwa mgombea pekee katika uchaguzi wa 2025 kwani umahiri na uhodari wake umeonesha kila mwanamke anaweza kuwa rais nchini.

# KAMPENI YA UIBUAJI WA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU

NA MUHIDIN AMRI, TUNDURU

WIZARA ya Afya kupitia mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Ki kuu na Ukoma imesema, kampeni ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kiku u itawafikia watu wote walioba inika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo ambao hawakufikiwa mwaka 2024.

Watu hao, wataanzishiwa Dawa ha raka kwa ajili ya kuzuia uweze kano wa kuambukiza watu wengin e ili kuifanya Tanzania kuwa nchi salama bila kuwa na watu walioambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu ifikapo mwaka 2 030.

Hayo yamesemwa jana na Mwakili shi wa Wizara ya Afya kitengo cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma Dkt Jacob Mwanamtwa, baada ya kukagua utekelezaji wa kampeni hiyo katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma.

Alisema, Wizara ya Afya imejipa nga na itahakikisha inawapata wagonjwa ambao hawakupatikana mwaka 2024 na kuwaanzishia matibabu yanayotolewa bure kwenye vituo vya Afya na Hospitali zote hapa nchini.

"Wagonjwa ambao hawajapatiwa m atibabu wanaendelea kuambukiza watu wengine katika jamii yetu na mbaya zaidi mgonjwa ambaye hajaanza kutumia Dawa anaweza kuambukiza watu kati ya 10 hadi 15 kwa mwaka" alisema Dkt Jacob.

Alisema, wameanza kampeni hiyo kwenye mikoa tisa hapa nchini ambayo haikufanya vizuri katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu mwaka jana ikiwemo Mkoa wa Ruvuma na kupitia kampeni hiyo wagonjwa wote watafikiwa ili waweze kuanzish iwa matibabu.

Alisema, malengo ya Shirika la Afya Duniani(WHO) kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030 , lakini kutokana na changamoto mbalimbali yanaweza yasifikiwe au yakafanikiwa kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali yetu kupitia Wizara ya Afya.

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukom a wa Wilaya ya Tunduru Dkt Mkasange Kihongole alisema, kupitia kampeni ya mpango harakishi watahakikisha wananchi wote wanapata elimu ya kifua kikuu, wanafanyiwa

***Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.***



uchunguzi na ambao watabainika kuwa na vimelea vya ugonjwa huo wataanzishiwa dawa.

"katika kipindi hiki cha mpito ambacho tunatakiwa kufanya kazi kwa juhudi kubwa tumeanza kuangalia maeneo hatarishi zaidi, baada ya hapo wataalam tutasambaa kwenye maeneo mengine ambayo siyo hatarishi lakini kuna watu ambao wako kwenye hatari ya kupata ugonjwa huo"alisema Mkasange.

Mkasange ametaja maeneo hatari shi ni kwenye maboma ya wafuga ji, vijiwe vya boda boda, wachez a bao, Pooltable machimbo ya madini na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu kuanzia watano na kuendelea.

Aidha alisema, kabla ya Wizara ya Afya kuzindua mpango haraki shi wa kuibua wagonjwa wa TB, Wilaya ya Tunduru imeshaanza kutekeleza kampeni hiyo kwenye vijiji vyote vinavyozun gukwa na machimbo ya madini, shule za Msingi na Sekondari za bweni.

Mkasange alisema, walianza kamp eni ya uelimishaji, uibuaji na uchunguzi wa TB mapema ili kwenda na kasi ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu iliyozinduliwa wiki iliyopita ili kukata mnyororo wa maambukizi katika wilaya ya Tunduru.

Naye Mratibu wa huduma za maab ara Mkoa wa Ruvuma Said Kaunde alisema, kampeni ya mpango harakishi ya uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu imegawanyika kwenye makundi mawili ambayo ni kuwafikia Wananchi wenye vimelea vya TB kwa ajili ya kuchukua sampuli za makohozi na kuwaanzishia Dawa.

Alisema, katika mkakati wa kuto komeza ugonjwa huo Serikali yetu imewekeza fedha nyingi kwenye vifaa tiba hasa kununua mashine za kisasa za uchunguz i wa vimelea vya kifua kikuu na katika Mkoa wa Ruvuma kuna mashine 11 ambazo zimepelekwa kwenye Halmashauri zote nane.

Pia alisema, tangu kampeni hiyo ilipoanza hadi sasa wamefanik iwa kukusanya sampuli zaidi ya 851 ambazo baada ya kupelekwa maabara kwa ajili ya uchunguzi,24 zimekutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.

Nyuki, ameipongeza Serikali kup itia Wizara ya Afya kwa kuchuk ua hatua katika kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni miongoni mwa magonjwa kumi Ulimwenguni yanayoongoza kusababisha vifo vya watu wengi.



# WIMBO 'KAKA SELEMANI' WA MSONDO! UMETIMIZA MIAKA 48 KAMA CCM



NA MWANDISHI WETU

1973 ulikuwa mwaka mzuri kwa Bendi ya NUTA jazz, si wanamuziki pekee bali hata wafanyakazi wa Muungano huo wa Wafanyakazi walipagawishwa na ujio wa mwimbaji kijana sana aliyejiunga na bendi mwaka huo.

Huyo ndiye Hassan Rehani Super Stereo aliyejiunga na bendi hiyo awali akidharauliwa kutokana na umri wake, lakini pale alipokaribishwa jukwaani bendi ilitikisika

Alipotinga Dar akitokea Arusha kwa ajili ya majaribio aliikuta bendi inajiandaa kusafiri kwenda Dodoma.

Viongozi wakaamuru na Bitchuka naye awemo katika msafara huo wa Treni ili wakamjaribu kama atafaa au hatakuwa na tija.

Mwenyewe alikuwa na Siri kubwa moyoni, akijipanga kuwanyamazisha pindi watakapompa nafasi, pengine aliyekuwa akifahamu makjali yake ni kaka yake na rafiki Said Mabela waliowahi kufanya kazi pamoja Arusha Jazz.

Naam saa na dakika zikatimia bendi ikafika salama na muda wa usiku ikaanza kutumbuiza katika ukumbi wa Dodoma Hotel huku Bitchuka akifuatilia kila tukio.

Hatimaye muziki ukazimwa na kutangazwa uwepo wake pia akatakiwa kupanda jukwaani ili kusalimia kisanii.

Lilikuwa kosa kubwa kwani mwamba huyo alipokabidhiwa kipaza sauti akafanya balaa kubwa akiimba wimbo maarufu wenye maneno "Ukiwa kama hunitaki"

Sauti yake ya juu, jinsi alivyoweza kuimba kama pacha na mwimbaji kinara Muhimu Gurumo ilimpagawisha kila aliyekuwemo ukumbini pamoja na wanamuziki wenzake, aliposhuka jukwaani saa hiyo hiyo ikapigwa simu Dar es Salaam akiagizwa Boss kuandaa haraka mkataba wa kijana huyo.

Bitchuka akafikia kusaini na kuanza kazi pia akipewa nafasi ya kuachia kibao chake cha kwanza na yeye akaamua kurudisha shukran kwa mashabiki kwa kutunga kibao kiitwacho 'Msondo wa NUTA'.

Kuanzia hapo kila aliyetaka kutunga wimbo basi pia alitamani kusikia Bitchuka akiimba na hiyo ikadumu kwa kipindi kirefu sana akiitumikia bendi hiyo kutoka 1917 hadi 1979 alipohamia Mlimani park.

Yote tisa, Kumi ni Katia tukio la bendi kutoka kuitwa NUTA na kuwa Juwata, baada ya kuunganishwa vuyama vya TANU na ASP mwaka 1977 bendi hiyo nayo mikakumbwa na mabadiliko hayo ya jina tu lakini wanamuziki ni walewale.

Wanamuziki wakapanga kutunga vibao hatari vitakavyoshabihiana na mabadiliko ya ya jina la bendi.

Naam ilipofika mwisho mwisho wa mwaka hupo Tarehe 11.11.1977 Mabrok Khalfan akatunga wimbo wenye mahadhi ya rumba na wenye miondoko ya taratibu pia akataka Bitchuka atambae katika sauti tamu ya Kwanza.

Wimbo huo ukawa katika albam yenye wimbo Nidhamu ya kazi ambao nao ulikuwa wenye viewango vya Lami.

Albam hii ilileta mtikisiko wa hali ya juu kwa mashabiki kuongezeka Msondo kiasi cha kuhitajika nguvu ili uweze kupata tiketi mapema ili uingia kufaidi midundo ya Msondo Ngoma.

Au ukizubaa utaingia ukumbini lakini hutoweza hata kuwaona wanamuziki.

Kutokana nyomi linavyojazana.

# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka




MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

ARSENAL wako tayari kuvunja rekodi yao ya uhamisho msimu wa kiangazi kwa dau la £100m (euro 120m) kumnunua mshambuliaji wa Inter Milan na Argentina Lautaro Martinez, mwenye umri wa miaka 27. (Fichajes - In Spanish)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## SIMBA YAKATAA OFA KWA KIBU DENIS

NA MWANDISHI WETU

BAADA YA kuikabili wenyeji wao Foutain Gate katika uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani Manyara, Wekundu wa Msimbazi wamekataa kumuuza nyota wao, Denis Kibu, kwa MC Algers ya Algeria, imefahamika.

Mechi huo ulikuwa wa tisa kwa Simba kushuka nje ya uwanja wake wa nyumbani, ambapo katika michezo nane imepata ushindi wa asilimia 100.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, aliliambia gazeti hili, timu yake imejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu ili kuendeleza kutoa dozi katika kila inapocheza ugenini msimu huu.

Kocha huyo alisema Simba imekuwa na matokeo mazuri inapocheza ugenini na hii inachagizwa na idadi kubwa ya mashabiki wanaojitokeza viwanjani kuwashangilia wachezaji wao.

"Nilisema na narudia tena, tunashinda sana ugenini kwa sababu tunacheza mechi za mikoani kama tupo nyumbani kutokana na kushangiliwa na mashabiki wengi zaidi kuliko wapinzani wetu ambao ni wenyeji, natarajia mechi hii itakuwa hivyo hivyo, na sisi tutawapa na kuwaachia mashabiki furaha ya ushindi, tukichukua pointi tatu na kurejea nazo Dar es Salaam," alisema Fadlu.

Hata hivyo, Simba inaweza kumkosa winga wake tegemeo, Kibu, aliyeumia katika mchezo uliopita, ingawa daktari wa timu, Edwin Kagoba, amesema hali yake inaendelea vizuri.

"Yuko katika hatua ya pili ya matibabu, tunategemea, atakapopita kwenye hatua zote za matibabu anaweza kuwapo kwenye mchezo wetu ujao. Ila hii uwepo wake ni nusu kwa nusu, kuna vitu tunaviangalia leo (jana) na kesho (leo), lakini niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Simba hali yake si mbaya si ya kumweka nje muda mrefu," alisema daktari huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate, raia wa Kenya, Robert Matano, amesema amekiandaa vyema kikosi chake kushindana na Simba, ingawa anaamini watawapa upinzani mkali.

# Michezo Kimataifa




# DAVIES MWAPE ALIPELEKA MAJONZI MSIMBAZI 2011

NA HENRY PAUL

MIONGONI mwa matukio yaliyowahi kuwafurahisha wanachama na wapenzi wa klabu ya Yanga, moja ni lile la timu yao yenye maskani yake makuu Kariakoo, makutano ya mitaa ya Jangwani na Twiga, kumfunga mtani wake wa jadi Simba bao 1-0.

Mchezo huo ambao ulikuwa ni mkali na wa kusisimua kwa muda wote wa dakika 90, ulichezwa siku ya Jumamosi Oktoba 29, 2011, katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru) na ulikuwa ni wa mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezo ulianza kwa kasi, huku timu zote zikishambuliana kwa zamu. Yanga walikuwa wanashambulia na pindi Simba nao walipokuwa wanapata nafasi walikuwa wanashambulia pia.

Mabeki wa timu zote mbili walikuwa makini mno katika kudhibiti mashambulizi yaliyokuwa yakielekezwa langoni mwao, huku washambuliaji nao walikuwa wakifanya mashambulizi kadhaa wakiwa na lengo la kutaka kupata bao la mapema mapema.

Mashambulizi ya Yanga, yalikuwa yakiongozwa na Davies Mwape, Kenneth Assamoah na Amisi Kiza, huku mashambulizi ya Simba yalikuwa yakiongozwa na Felix Sunzu, Emmanuel Okwi na Ulimboka Mwakingwe.

Kosa kosa za kutaka kufunga zilikuwa zikitokea pande zote mbili, kwa sababu mabeki walionekana kuwa imara katika kudhibiti mashambulizi ya washambuliaji.

Katika dakika ya 30 hivi, Simba walifanya shambulizi moja kali langoni mwa timu ya Yanga, lakini shuti hafifu alilopiga Emmanuel Okwi, lilidakwa kirahisi na kipa wa Yanga Yaw Berko.

Yanga ilijibu shambulizi hilo katika dakika ya 32 hivi, baada ya kiungo wao mahiri Haruna Niyonzima kutoa pasi kwa Kenneth Assamoah, lakini shuti lake lilitoka sentimita chache langoni mwa timu ya Simba.

Dakika ya 40 hivi, Simba walifanya shambulio lingine kali langoni mwa timu ya Yanga, lakini Sunzu aliyecheza vizuri siku hiyo, alikosa bao la wazi baada ya kubaki yeye na kipa wa Yanga Berko, kwani shuti lake kali alilopiga lilitoka nje kabisa.

Hadi dakika 45 za kipindi cha kwanza zinamalizika, timu hizo zilikwenda mapumziko matokeo yakiwa ni suluhu ya 0-0.

Kipindi cha pili nacho kilianza kwa kasi, huku timu zote mbili zikifanya mabadiliko ya wachezaji wao. Katika dakika ya 50, Simba ilimpumzisha Amri Kiemba na nafasi yake kuchukuliwa na Haruna Moshi 'Boban'.

Kuingia kwa kiungo mashambuliaji 'Boban', kwa kiasi fulani kuliongeza kasi ya mashambulizi kwa upande wa Simba, kwani walionekana kufanya mashambulizi mengi langoni mwa timu ya Yanga tofauti na mwanzoni.

Yanga kwa kutaka kuongeza mashambulizi mbele, katika dakika ya 55, ilimtoa Amis Kiza na nafasi yake kuchukuliwa na Idrisa Rashid ambaye baada ya kuingia alioneza kasi ya mashambulizi kwa timu yake ya Yanga.

Dakika ya 70 hivi, Simba ilimtoa winga wa kushoto Ulimboka Mwakingwe na nafasi yake kuchukulia na Mwinyi Kazimoto.


Katika dakika ya 75 hivi, Yanga walifanya shambulio moja la nguvu langoni mwa timu ya Simba na kufanikiwa kupata bao la kuongoza ambalo lilifungwa na Davies Mwape.

Dakika ya 80 hivi, Yanga ilifanya badiliko lingine kwa kuingia Jerry Tegete aliyechukua nafasi ya mfungaji wa bao pekee Davies Mwape.

Pamoja na mabadiliko ya wachezaji kufanywa na pande zote, lakini hapakuwa na mabadiliko ya matokeo, hivyo hadi dakika 90 za mchezo zinamalizika, Yanga walitoka uwanjani wakiwa vifua mbele baada ya kumfunga mtani wake wa jadi Simba bao 1-0.

Kikosi cha Yanga: Yawa Berko, Godfrey Taita, Oscar Joshua, Chacha Marwa, Nadir Haroub 'Cannavaro', Juma Seif 'Kijiko', Nurdin Bakari, Haruna Niyonzima, Davis Mwape/Jerry Tegete, Kenneth Assamoah na Amis Kiza/Idrisa Rashid.

Kikosi cha Simba: Juma Kaseja, Said Nassor 'Chollo', Juma Jabu, Juma Nyoso, Victor Costa 'Nyumba', Jerry Santo, Amri Kiemba/Haruna Moshi 'Boban', Shomari Kapombe, Felex Sunzu, Emmanuel Okwi na Ulimboka Mwakingwe/Mwinyi Kazimoto.



JAMVI LA HABARI
# SPOTI
IJUMAA FEBRUARI 07, 2025



## Diamond athibitisha Mbosso kusepa WCB

>> Soma Uk. 15

# SIMBA YAVUTWA MKIA NA MANYARA



NA MWANDISHI WETU

TIMU ya Simba hatimaye imeendelea kukaa nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania ya NBC baada ya jana kuambulia pointi moja katika mchezo wa ligi hiyo ilipocheza dhidi ya Fountain gate na kupata sare ya bao 1-1.

Licha ya kumiliki mchezo huo kwa vipindi vyote, Simba ilijikuta ikiambulia matokeo hayo baada ya kosa kubwa la kiungo wake Ladack Chasambi aliyejifunga baada ya kuurejesha mpira golini kwa shuti kali lililomshinda kipa Moussa Camara na kuukwamisha wavuni.

Bao la Simba lilifungwa na Leonel Ateba aliyewekewa pande zuri na Chasambi na kukwamisha mpira huo kimiani katika dakika ya 57.

## Homa ya AFCON yapamba moto Afrika mashariki

NA MWANDISHI WETU

HOMA ya kufanyika kwa michuano ya AFCON katika nchi za Afrika Mashariki Uganda, Kenya na tanzania kunaendelea kupasua vichwa vya mashabiki wa soka, wanaojali tukio hilo kubwa la kihistoria.

Michuano hiyo itafanyika kwa ushirikiano wa nchi hizo ambazo ndiyo waandaji, huku kilka nchi ikieendelea na ujenzi pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ili kuhakikisha michezo hiyo inafanyika bila vikwazo



Waziri anayeshugulikia michezo nchini Kenya Salim Mvurya amekuwa na kibarua kizoyto cha kusimamia maandalizi hayo usiku na mchana, huku Waziri mdogo katika Wizara ya Elimu na michezo anayeshuguliksia eneo hilo nchini Uganda Peter Ogwang naye akieleza kujridhishwa mna maandeleo ya maandalizi ya michuano hiyo.

Nchini tanzania hivi karibuni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alisema Serikali imejipanga vyema kukamilisha maandalizi yote muhimu ikiwemo miun-

>> Inaendelea Uk. 14



## Simba yakataa ofa kwa Kibu Denis

BAADA YA kuikabili wenyeji wao Foutain Gate katika uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani Manyara, Wekundu wa Msimbazi wamekataa kumuuza nyota wao, Denis Kibu, kwa MC..

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM